**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UDHIBITI WA USALAMA WA VYOMBO VYA MOTO KIBIASHARA

**Ndugu Wanahabari,**

**Watoa Huduma wa Usafiri wa Umma na Mizigo Kibiashara,**

**Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini**

**Wadau Wetu Wote na Wananchi kwa Ujumla,**

**Mabibi na Mabwana, Itifaki Imezingatiwa,**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, afya njema na fursa ya kukutana tena ili tuweze kupeana taarifa muhimu katika eneo tunalosimamia nanyi mtusaidie kuuhabarisha umma wa Watanzania.

Niwashukuru sana nanyi kwa kuitikia mwaliko wetu kuwepo hapa. Kalamu yenu ni ya wino wa dhahabu ambayo kwetu ina thamani kubwa sana. Hivyo, tutumie vyema kalamu zetu kufikisha ujumbe utakaojenga Taifa bora lenye amani, umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa Watanzania. Asanteni sana.

Aidha, nitumie fursa hii kutoa Pongezi za dhati kwa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Uongozi wake Mahiri wenye mafanikio lukuki katika Awamu hii ya Sita. Kwa uchache niseme Uongozi wa Mhe. Rais katika Awamu hii, imetujengea mazingira mazuri na bora ya kusimamia sekta hii katika eneo letu. Haya pia yamekuwa mepesi sana kwetu kutokana na Uongozi mahiri na madhubuti wa wasaidizi wake hususan Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi na Uchuchuzi na Manaibu Mawaziri wake pamoja na Bw. Gabriel Migire, Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi.

Pia niwashukuru sana wadau wetu wote hasa watoa huduma na watumiaji wa huduma. Tumekuwa tukipata ushirikiano mkubwa toka kwa wamiliki wa vyombo vya moto vinavyofanya kazi zao kibiashara. Hii ni pamoja na watoa huduma mmoja mmoja lakini pia kupitia vyama vyao (mf. TABOA, TAT, TATOA, TAMSTOA). Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wao, ukaribu wao na Mamlaka yetu na tunaendelea kuwaomba pale wanapo kwazika na udhibiti wetu, milango yetu na Serikali kwa ujumla ipo wazi. Njooni tuongee na tuboreshe penye mapungufu. Jukumu letu ni kuwasaidia wakuze mitaji yao waliyowekeza na kuboresha huduma kwa wananchi.

Baada ya Shukrani hizo, nitaoe taarifa muhimu zifuatazo:

## 1. Kuwepo kwa Ukiukwaji wa Maadili ya Kitanzania

Kumekuwa na taarifa la ongezeko la ukiukwaji wa maadili ya Tanzania kwenye vyombo vya usafiri wa umma. Hali hii inatokana na wamiliki wa vyombo hivyo kutokuwa na wasimamizi madhubuti na weledi wa Kanuni za Usafiri wa Umma za Mwaka 2020. Tumeshatoa matamko kadhaa kukumbusha mazuio ya Kikanuni mf. Kufanya biashara, mahubiri ya dini na kuweka picha za video na miziki isiyo na maadili ya Kitanzania.

Leo nakumbusha tena na ninasisitiza kila mmiliki azingatie Kanuni hizo. Mkazo wangu kwa siku ya leo ni kwenye video na miziki isiyo na maadili kwenye mabasi. Hapa tutashirikiana na Baraza la Filamu Tanzania na tutachukua hatua stahiki.

Kwa sasa kila mtoa huduma aanze kutathmini video na miziki inayopigwa kwenye magari yake endapo akikaa na mwanae, mzazi wake nk anaweza kuziangalia au kuzisikiliza.

Lakini kingine, kumekuwa na matukio ya kuwafanyia vitendo vya kikatili wanafunzi hasa wa kike kwenye mabasi ya Shule, na zipo taarifa za wanafunzi hawa kunajisiwa. Jambo hili halivumiliki na halikubaliki kwa ustaarabu wetu na umma huu wa Watanzania. Kwa sasa tunaelekeza, Shule zote ziwasilishe Orodha ya Mabasi yanayotoa huduma kwa shule husika na majina ya madereva, namba za leseni na NIDA. Aidha, kila shule iwasilishe orodha ya wahudumu wa mabasi hayo (matroni na patroni) na namba zao za NIDA. Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inafanya mapitio ya Kanuni za Usafiri wa Umma ili kuongeza vigezo vya udhibiti wa mabasi ya shule.

## 2. Marekebisho ya Kanuni za Usafiri wa Kukodi

Serikali imefanya marekebisho madogo kwenye Kanuni za Usafiri wa Kukodi za Mwaka 2020 (The Land Transport Regulatory Authority (Private Hire Services) Regulations, 2020) na kuruhusu utaratibu wa kujidhibiti wenyewe (self-regulation) na uwepo wa Wakala aliyeidhinishwa (Authorized Agent) katika utoaji wa leseni za huduma hizo. Hasa itahusu pikipiki (bajaji na bodadoba) kwa utaratibu wa vyama vya ushirika (SACCOS). Aidha, itaruhusu mwakala binafsi na Taasisi za Umma.

Marekebisho haya yamefanyika na kuridhiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge la Sheria Ndogo na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali tarehe 31 Machi, 2023 **(GN. No. 254 of 2023).**

## 3. Kusitisha Leseni za Mabasi Yendayo Mikoani

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inautaarifu umma kuwa imesitisha leseni za usafirishaji abiria kwa mabasi 27 kwa kipindi cha mwezi Machi, 2023. Uamuzi huu umefanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(b) ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 na Kanuni ya 27(1)(c) na (d) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020.

Hatua hii ni kutokana na vitendo vya kuingilia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kusababisha **mfumo kutotuma taarifa kabisa** ama **kutuma taarifa kwa kurukaruka** (skipping). Hapa kuna baadhi ya mabasi ambayo baada ya wataalamu wa Mamlaka kufanya uchunguzi, waligundua betri za vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTDs) zimeharibiwa na mifumo yake ya umeme kubadilishwa. Kadhalika, kuna mabasi ambayo yamekutwa yakiwa na mfumo wenye swichi inayotumiwa na dereva kuzima na kuwasha kifaa hicho (VTD). Lakini kibaya na hatari Zaidi, yapo mabasi ambayo yamebadilishwa mfumo (software) na kutuma taarifa za uongo kwenye kituo chetu cha ufuatiliaji. Utaona basi linasafiri mpaka linafisha kwa spidi isiyobadilika. Hapa, ni muhimu wamiliki wa mabasi na madereva wafahamu kuwa mfumo wa VTS una uwezo wa kutoa taarifa kwa Mamlaka iwapo utaingiliwa au kuharibiwa.

Kitendo cha kuingilia Mfumo wa VTS ni ukiukwaji wa Kanuni ya 51(a) na (b) ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji (Magari ya Abiria) za Mwaka 2020. Kanuni ya 51(a) inamtaka mmiliki (mwenye leseni) ahakikishe basi lake limefungwa kifaa cha kufuatili gari (*installed with VTD*), kiwe kinafanyakazi vyema (*working properly*), kinafanyiwa marekebisho (*maintained*), kinakingwa na mazingira hatarishi (*protected against hazardous conditions*) na hakichezewi (*tempering*). Aidha, Kanuni ya 51(b) inaelekeza "kifaa chochote cha ufuatiliaji wa magari (VTD) kitakapokuwa hakifanyi kazi ipasavyo (*any malfunctions of VTD*) kitolewe taarifa kwa Mamlaka ndani ya saa 12 (*reported to the Authority within twelve hours*).

Hivyo, Mamlaka imechukua hatua ya kusitisha leseni za mabasi 27 (Orodha imeambatishwa-Kiambatisho 1) kwa mujibu wa Sheria ya LATRA, Sura ya 413 na Kanuni zake za Mwaka 2020. Katika barua zetu za kusitisha leseni hizi, tuliwaelekeza wamiliki wa mabasi husika, kabla hatujaondoa sitisho letu, wafanye marekebisho ya mfumo na kujiridhisha unafanyakazi vyema kisha wawasilishe uthibitisho wa marekebisho hayo. Pia tumewaelekeza kuwafikisha madereva husika Jeshi la Polisi kwa hatua zingine chini ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168.

## 4. Kuwasimamisha Watoa Huduma wa Vifaa vya Kufuatilia Mwenendo (VTDs)

Mamlaka ina Mkataba na Watoa Huduma watano (5) ambazo ni kampuni zilizochaguliwa kwa mchakato wa zabuni wa kufunga vifaa vya kufuatilia mwenendo wa magari (VTDs) ambao ni Fleet Truck, Tera Technologies, Easy Truck, Utruck na ICTPack.

Katika kutathmini utendaji kazi wao kwa mujibu wa Mkataba, Mamlaka ilibaini mapungufu kwa kampuni mbili (2) ambayo hayawezi kuvumilika.

Hivyo, Mamlaka imewasimamisha watoa huduma wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi ambao vifaa vyao vimebainika kuchezewa. Watoa huduma hao ni **Utrack Africa Ltd** na **Easy Track Solution JV RJ Motchand Ltd**. Kampuni hizi kwa sasa zinatakiwa kurekebisha kasoro zilizobainika kwenye mabasi yaliyofungiwa na wakikamilisha watarudishwa kuendelea na utoaji wa huduma ya kufunga vifaa vipya.

## 5. Kusitisha Leseni za Madereva

Katika mwezi Machi 2023, Kamanda wa Polisi – Kikosi cha Usalama Barabarani amewafungia leseni madereva 15 waliohusika kuharibu mfumo wa VTS ili mabasi yao yakimbie pasipo kuonekana. Majina ya madereva hao yameambatishwa kwenye taarifa hii (Kiambatisho Na. 2).

Ili kuboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo, LATRA inaendelea kuwasajili na kuwathibitisha madereva kwa mujibu wa Sheria ya LATRA Sura ya 413 kifungu namba 5(1)(e). Kwa mujibu wa masharti ya leseni za kutoa huduma ya usafirishaji, wamiliki wote wa vyombo vya Usafiri kibiashara wanatakiwa kuwa na madereva ambao wamesajiliwa na kuthibitishwa. Ili kusajiliwa, dereva anatakiwa kuwa na leseni hai ya udereva, cheti cha mafunzo ya udereva na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA). Dereva anaweza kusajiliwa popote alipo kwa kuwasilisha maombi kupitia anuani ya; https://rrims.latra.go.tz/login.

Mamlaka inawakumbusha wamiliki na madereva wote wa vyombo vya moto kibiashara kuhaikisha wamekamilisha usajili wa madereva ifikapo Aprili 30, 2023 kama ilivyotangazwa hapo awali.

## 6. Kuzingatia Sheria Katika Kutoa Huduma na Kuwasilisha Malalamiko

Tunawakumbusha wamiliki/watoa huduma ambao tumesitisha leseni za magari yao kuzingatia Sheria na Kanuni katika utoaji wa huduma hii kwa umma na kuwasilisha malalamiko.

Kazi yeyote utaifanya kwa umahiri na ubora endapo utazingatia Sheria na Kanuni inayoliongoza jambo hilo. Hivyo, tunawasihi waajiri watu weledi na wanasheria mahiri watakaoweza kuwasaidia kusimamia huduma hii na kuwashauri ipasavyo ili kuboresha huduma kwa wateja, kukuza mitaji na biashara zao. Wahakikishe matumizi ya tiketi za kielektroniki, huduma bora kwa wateja.

Mwisho, pale mnapoona maamuzi yetu kama Mdhibiti sio sahihi, Sheria inataka mje kwetu kupinga maamuzi hayo kwa hoja na kuna Jopo la Mapitio (Review Panel) ya Bodi itafanya kazi yake na kutoa maamuzi, Na endapo hujaridhika na maamuzi ya Review Panel, basi hatua inayofuata ni kwenda kwenye Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal). Hapa mwanasheria wenu wawasaidie msipoteze muda kwenye utaratibu usio rasmi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

CPA Habibu J. S. Suluo
Mkurugenzi Mkuu - LATRA
11 Aprili, 2023

**Kiambatisho 1. Orodha ya Mabasi Yaliyositishiwa Leseni.**

| Na. | Namba ya Basi | Mmiliki | Tarehe ya Leseni Kusitishwa |
|---|---|---|---|
| 1. | T717EBK | Maning Nice | 1.3.2023 |
| 2. | T568DVS | Machame Investment | 2.3.2023 |
| 3. | T291CJX | Simba Mtoto | 2.3.2023 |
| 4. | T423CVL | Godfrey Augustino Luhifa | 2.2.2023 |
| 5. | T437DQR | Geofrey Josiah Mushema | 2.3.2023 |
| 6. | T703DEG | Bujiku Wilson Tambalu | 2.3.2023 |
| 7. | T719DHU | Lucas Nyakabaka Limbu | 2.3.2023 |
| 8. | T754DPC | Mbaga Samwel Shitobelo | 2.3.2023 |
| 9. | T882DQE | Boniface Daima Ilomo | 2.3.2023 |

| Na. | Namba ya Basi | Mmiliki | Tarehe ya Leseni Kusitishwa |
|---|---|---|---|
| 10. | T985DPV | Emmanul Likinda Lutima | 2.3.2023 |
| 11. | T992DJW | Lubiga Investment | 2.3.2023 |
| 12. | T814DXN | BM Coach | 2.3.2023 na 3.4. 2023 |
| 13. | T919DCT | Bilo Star | 13.3.2023 |
| 14. | T423DTW | Baraka Classic | 15.3.2023 |
| 15. | T689EBD | Jacob Duka Malessa | 15.3.2023 na 28.3.2023 |
| 16. | T252AZU | Rahabu Logistic Company Limited (ABF) | 17.3.2023 |
| 17. | T216ABF | Mumuk Investment | 17.3.2023 |
| 18. | T821DTP | BM Coach | 17.3.2023 |
| 19. | T582EDL | BM Coach | 17.3.2023 |
| 20. | T367ARH | Asante Rabi | 17.3.2023 |
| 21. | T397AWM | Haji Mohamed Ahmed | 20.3.2023 |
| 22. | T233EBG | Yahaya Ally Amour (Ally's Star) | 20.3.2023 |
| 23. | T403DWH | Super Feo | 21.3.2023 |
| 24. | T712DPK | New Force | 22.3.2023 |
| 25. | T804DCE | Kapesa Benedict Mberesero | 25.3.2023 |
| 26. | T361EBS | Happy Nation | 31.3.2023 |
| 27. | T657 EBK | Happy Nation | 31.3.2023 |

**Kiambatisho Na. 2. Orodha ya Madereva Waliofungiwa Leseni kwa Kosa la Kuchezea Mfumo wa VTS na Mwendo Kasi**

1. ABDALLAH SALIM NASSORO
   D/L NO. 4000331020
   T.902 AGY -- ADVETURE
   KUCHEZEA VTS NA KUZIDISHA MWENDO

2. STEPHANO LAISON MWAMBOGOLO
   D/L NO. 4002007407
   T.653 DZY – (MMILIKI) GOODLUCK SHIRIMA
   MWENDOKASI

3. NTUNGWA MHY ASELE MASISA
   D/L NO. 4001395305
   T.323 DUF CONTINATAL EXPRESS
   MWENDO KASI / KUCHEZEA VTS

4. HAMISI SHABANI MKUNGI
   D/L NO. 4005123645
   T. 166 DQX MANNING NICE
   KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

5. YUSUPH T. YUSUPH
   D/L NO. 4001083269
   T. 995 DQW MANNING NICE
   KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

6. SHABANI DIWANI MAULIDI
   D/L NO.4000180 683
   T. 348 DFS KIDIA ONE INVESTMENT
   KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

7. ABDULMALIKI HAMIDU HASSAN
   D/L NO. 4000450337 KIDIA ONE INVESTMENT
   T.348 DFS
   KUCHEZEA VTS MWENDO KASI

8. JOHN  JOSEPH KIZONGO
   D/L NO. 4000180683
   T. 884 DEE BONGE EXPRESS
   KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

9. AWADHI SAID ALBAZEER
   D/L NO. 400361882
   T.447 CHQ SIMBA VIDEO
   KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

10. RAMADHANI SHABANI JAMES
    D/L NO. 4001307722
    KVC282R TAHMEED COACH
    KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

11. JOSEPH KATAMA RIKO
    D/L NO. 4000058574
    T.730DRN TAHMED COACH
    KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

12. RICHARD ELLO NZUNDA
    D/L NO. 4001472482
    T. 712 DK NEW FORCE
    KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

13. MAZOLA GRAYSON MWAMAFUPA

    D/L NO. 4000031689

    T.712DPK NEW FORCE

    KUCHEZEA VTS / MWENDO KASI

14. JUSTINE ALBERTO MTEGETE

    D/L NO. 4000424546

    T.403DWH SUPER FEO

    KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI

15. ABED ATHANA BAYAGA

    D/L NO. 4000266619

    T.919 DCT BILO STAR

    KUCHEZEA VTS/ MWENDO KASI